HOTUBA YA CSOs KATIKA UFUNGAJI WA MKUTANO WA 8 WA MWAKA WA TATHMINI YA SEKTA YA ELIMU MWAKA 2025

Mhe. Mgeni Rasmi

Waheshimiwa wote mlioshiriki katika Mkutano huu muhimu

Mabibi na mabwana Habari za Mchana

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Wakati tunamaliza safari hii ya siku tatu ya tathmini ya sekta ya Elimu (AJESR) ya mwaka huu 2025, napenda kuchukua fursa hii kutoa shuran za dhati kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa kuendeleza utamaduni huu kuwaalika wadau wa elimu kufanya tathimini ya upatikanaji wa ubora wa elimu Zanzibar. Pia nawashukuru washiriki wenzangu kwa ushiriki wenu wa hali ya juu, kwa mijadala ya kina, na kwa maoni yenye mchango mkubwa katika safari ya kuboresha elimu yetu Zanzibar

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kwa siku hizi chache tumeweza, kubadilishana mawazo na uzowefu, na kuangazia maendeleo tuliyoyapata kwa umoja wetu.

Katika tathmini hii imebainika kwamba mafanikio ni makukwa licha ya changamoto zilizopo ambazo mkutano huu umezipatia mapendekezo ya kuzipunguza au kuziondoa kabisa.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi

CSOs tunaamini kuwa hata baada ya kikao hiki kufungwa, kazi yetu haijafika mwisho. Maazimio tuliyokubaliana yanahitaji kuchukuliwa kwa uzito, kutekelezwa kwa wakati, na kufuatiliwa kwa karibu. Hatua za utekelezaji lazima ziwe na mwelekeo wa wazi, zenye uwajibikaji, na zinazoleta mabadiliko ya kweli kwa wanafunzi wetu.

Tunapaswa kuendelea kujifunza kutoka kwa kila mmoja wetu, kukuza ubunifu, na kushirikiana kwa karibu zaidi katika utekelezaji wa maazimio hayo.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi

**MAPENDEKEZO**

1. Sera ziboreshwe ili kuwatambue na kuwaendeleza watoto wenye vipaji

2. Serikali na Washirika wa maendelea waeke nguvu ya fedha katika sekta binafsi - kwani nao wanajenga jamii moja.

3. Serikali iwajengee mazingira na motisha walimu wanaojitolea kujiendeleza kiutaalamu wa kufundisha na kutumia muda wa ziada kwa kwa ajili ya kuboesha uwezo wao wa kufundisha.

4. Pamoja na hatua na mahusiano mazuri yaliofikiwa baina ya skuli binafsi na wizara ya elimu - wizara ishirikishe skuli binafsi katika maamuzi muhimu yanayowahusu, badala ya kutoa maagizo tu.

Kwa dhati kabisa tunapenda kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uongozi thabiti na dhamira ya dhati katika kuboresha elimu. Pia tunawashukuru washirika wa maendeleo kwa msaada wao endelevu, kifedha na kiufundi. Tunawashukuru pia Wataalamu wa elimu, walimu, na washiriki wote kwa maarifa, uzoefu na michango yao yenye thamani kubwa kwa uimarishaji wa sekta ya Elimu Zanzibar

Mwisho, niwashukuru wana sekretarieti ya AJESR kwa kuratibu vizuri shughuli hii Muhimu